

Tiba ya ukoma inachukua miezi sita hadi mwaka mmoja kulingana na aina ya ukoma.

Tiba ya miezi sita: Tiba hii ni vidonge ambavyo humezwa kila siku na mgonjwa mwenye ukoma hafifu (PB). Mgonjwa wa aina hii ya ukoma analazimika kuonana na mhadumu wa afya mara moja kila mwezi ili aweze kupimwa na kupewa dawa zake za mwezi mzima.

Tiba ya miezi kumi na miwili (mwaka mmoja): Tiba hii ya vidonge humezwa kila siku na mgonjwa mwenye ukoma mkali (MB). Mgonjwa wa aina hii ya ukoma analazimika kuonana na mhadumu wa afya mara moja kila mwezi ili aweze kupimwa na kupewa dawa zake za mwezi mzima.

Tiba ya Ukoma hutolewa bila malipo katika vituo vyote vya tiba nchini

Mgonjwa ambaye ameanza tiba hawezi kumuambukiza mtu mwingine na hivyo hakuna sababu ya kumtenga na anaweza kuendelea na shughuli za kawaida za maisha.

HALI INAYOWEZA KUJITOKEZA WAKATI WA TIBA:-

- Mkojo kuwa mwekundu
- Ngozi kuwa nyeusi na kupauka

Endapo mojawapo ya hali hizi ikijitokeza usiogope, baada ya matibabu hali hurudi kama kawaida.

KUMBUKA !

- Ukoma siyo ugonjwa wa kulogwa wala kurithi
- Ikiwa utawahi na kugundulika una ukoma unatibiwa na kupona kabisa hivyo kuzuia ulemavu utokanao na ukoma.
- Mshauri ndugu/jamaa yako mwenye dalili kama zilizotajwa hapo juu kuwahi kwenye kituo cha tiba kwa vipimo na matibabu.

Uhusiano kati ya kifua kikuu na ukoma

Magonjwa ya kifua kikuu na ukoma husababishwa na vimelea ina ya bakteria wa jamii ya "mycobacteria" na maambukizo ni kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mtu mwingine.

Vimelea vya kifua kikuu huzaliana katika mapafu na kuenea katika viungo vingine, na vile vya ukoma hushambulia mishipa ya neva na ngozi. Ukubwa wa madhara ya kifua kikuu na ukoma hutegemea kiwango cha kinga mwilini.



Kwa maelezo zaidi wasiliana na mtoa huduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

kupitia

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma

S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.

Barua pepe: info@moh.go.tz,

Tovuti: www.ntlp.go.tz,

Toleo la 2016



**Fahamu Ukweli
Kuhusu Ugonjwa wa**

KIFUA KIKUU / UKOMA

UKOMA NI NINI?

Ukoma ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea ambavyo huathiri ngozi na mishipa ya fahamu.



JINSI UKOMA UNAVYOENEA

Ukoma huenezwa kawa njia ya hewa. Chanzo cha maambukizi hayo ni mgonjwa wa ukoma ambaye hajaanza matibabu. Mgonjwa huyo akipumua au kupiga chafya husambaza vimelea hivyo kwenye hewa.

AINA ZA UKOMA

Kuna aina mbili za ukoma:

1) Ukoma hafifu(PB): Ukoma wenye vimelea vichache.

Hii ni aina ya ukoma unaowapata watu wenye kinga kubwa dhidi ya ukoma. Ukoma huu una vimelea vichache sana na mgonjwa mwenye

aina hii ya ukoma haambukizi ugonjwa wa ukoma. Aina hii ya ukoma ina mabaka machache yasiyozidi matano.

2) Ukoma Mkali(MB): Ukoma wenye vimelea vingi.

Hii ni aina ya ukoma unaowapata watu wenye kinga ndogo dhidi ya ukoma. Ukoma huu una vimelea vingi na mgonjwa mwenye aina hii ya ukoma huambukiza ugonjwa wa ukoma katika jamii kwa njia ya hewa iwapo hajapata matibabu. Ukoma huu mkali una mabaka zaidi ya matano pamoja na dalili nyingine zote za ukoma.

DALILI ZA UKOMA

A: Dalili za awali:

1. Baka au mabaka yasiyo na hisia, yenye rangi ya shaba na hutokea sehemu yoyote mwilini. Baka au mabaka yanaweza kuwa bapa au yaliyovimba, hayawashi, hayaumi na hukosa hisia ya mguso.
2. Kuvimba au kuuma kwa mishipa ya fahamu ya mikono, uso na miguu na pengine mshipa mkubwa wa fahamu wa shingoni.

B: Dalili kamili:


1. Kuwepo kwa dalili zote changa.
2. Kuvimba vinundu kwenye masikio na na sehemu nyingine za mwili.

3. Ganzi kwenye mikono au miguu au vyote.
4. Kuwepo kwa vidonda visivyoyuma mikononi na miguuni.
5. Kushindwa kufumba jicho au macho.
6. Kuishiwa nguvu kwa misuli na kukakamaa kwa viganja vya mikono na miguu.
7. Kuvimba mwili kukiambatana na homa kali
8. Kupoteza baadhi ya viungo vya mwili kama vile vidole vya miguu au mikono.
9. Kuwepo upofu.

Dalili zote hizi zinaashiria kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa ugonjwa wa ukoma. Mara uonapo dalili hizi, unashauriwa kufika katika kituo cha tiba kilichopo karibu nawe kwa uchunguzi.

TIBA YA UKOMA

Ugonjwa wa ukoma hutibiwa kwa mchanganyiko wa dawa maalum zilizokanazwa kitaalamu kama "Multi drug therapy" (MDT) zilizowekwa kwenye pakiti.



Kila pakiti moja ya dawa ina vidonge vya kutosha siku ishirini na nane (28). Katika pakiti hiyo kuna dawa za kunywa mara moja kwa mwezi chini ya uangalizi wa mhudumu wa afya na nyingine za kila siku nyumbani.